# Jinsi ya kupiga ura katika uchaguzi mkuu wa jimbo la Vermont wa 2024

Uchaguzi mkuu wa Vermont unafanyika Jumanne, terehe 5 Novemba.

## Kuna njia mbili za kupiga kura:

1. Kupiga kura mapema kupitia barua ya posta au kwenda mwenyewe, kuanzia tarehe 1 Oktoba hadi tarehe 4 Novemba.
2. Kwenda mwenyewe katika kituo chako cha kupiga kura tarehe 5 Novemba.

Raia wote wa Marekani wanaoishi katika jimbo la Vermont na ambao watakuwa na umri wa miaka 18 au zaidi kufikia wakati wa uchaguzi mkuu utakaofanyika tarehe 5 Novemba, 2024 wanaweza kujisajili kupiga kura katika uchaguzi huo.

## Usajili wa wapiga kura

Ili kupiga kura katika uchaguzi mkuu, ni lazima uwe umesajiliwa kupiga kura katika jimbo la Vermont, ingawa unaweza pia kujisajili katika siku ya uchaguzi.

Ikiwa hujasajiliwa, kuna njia kadhaa za kujisajili:

- Kwenda mwenyewe katika ofisi ya karani wa mji wako siku kadhaa kabla ya uchaguzi.
- Kwenda mwenyewe kwenye kituo chako cha kupigia kura. Unaweza kujisajili katika kituo chako cha kupiga kura katika siku ya uchaguzi (tarehe 5 Novemba).
- Unaweza pia kujisajili mtandaoni au kupitia posta ukitumia fomu ya kujisajili ya karatasi; njia hizi mbili zinapatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya

Katibu wa Jimbo (bit.ly/4cKKLU8), lakini hakikisha unaacha siku kadhaa ili usajili wako uchakatwe ikiwa unatumia njia hizi.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Katibu wa Jimbo (bit.ly/4cKKLU8), watu wanaojisajili kwa mara ya kwanza watatakiwa kuwasilisha nakala ya kitambulisho halali. Hati zinazokubalika ni pamoja na:

- Kitambulisho halali chenye picha (leseni ya udereva au pasipoti)
- Bili ya sasa ya huduma ya matumizi
- Taarifa ya sasa ya benki
- Hati nyingine iliyotolewa na serikali

Watu wanaopiga kura kwa mara ya kwanza katika jimbo la Vermont sharti pia wale kiapo cha wapiga kura. Hii ni kauli fupi ambayo mtu anaweza kutamka mwenyewe.

## Kupiga kura mapema

Upigaji kura wa mapema unapatikana kuanzia tarehe 1 Oktoba hadi tarehe 4 Novemba. Kuna njia kadhaa za kuomba na kuwasilisha karatasi yako ya kupigia kura.

- Tuma ombi la kupata karatasi yako ya kupigia kura:
  - Kwa kwenda mwenyewe kwenye ofisi ya karani wa mji wako AU
  - Mtandaoni au kupitia posta ukitumia fomu ya kujisajili ya karatasi inayopatikana kwenye tovuti ya Ofisi ya Katibu wa Jimbo (bit.ly/3yPmu1j).
- Kisha, wasilisha karatasi yako ya kupigia kura:
  - Kwa njia ya posta AU

- Ipeleke katika ofisi ya karani wa mji wako.

Karatasi za kupigia kura za mapema ni lazima zipokewe katika ofisi ya karani wa mji wako kufikia mwisho wa saa za kazi mnamo tarehe 4 Novemba. Ikiwa unatuma karatasi yako ya kupigia kura kwa posta, itume kufikia tarehe 28 Oktoba ili kuruhusu wiki moja ya kuisafirisha.

## Siku ya Uchaguzi

Ili kupiga kura wewe mwenyewe mnamo tarehe 5 Novemba: Tafuta kituo chako cha kupigia kura kwenye tovuti ya Ofisi ya Katibu wa Jimbo (bit.ly/4g4prvC). Upigaji kura utaanza katika nyakati tofauti kuanzia saa kumi na moja asubuhi hadi saa nne asubuhi na kukamilika saa moja jioni.